


Bi Kizee alikuwa na mjukuu
aliyeitwa Noah.

Alimpatia Noah yai.



Noah alikutana na wachuma matunda damu.

Walilivunja yai hilo.



Noah alilia, “Yai lilikuwa la kulipia mahari!”



Wachuma matunda damu
walimpatia Noah fimbo.



Noah aliwakuta wajenzi.

Wakaivunja fimbo ile.



Noah akalia, “Fimbo hiyo ilikuwa ya wachuma matunda damu!”



Wajenzi walimpatia Noah kifurushi cha nyasi.



Noah akamkuta mchungaji
wa ng'ombe.

Ng'ombe akaila nyasi hiyo.



Noah alilia tena,
“Ile nyasi ilikuwa ya
wajenzi!”



Mchungaji alimpatia Noah
ng'ombe.



Noah alipata sherehe ya
harusi.

Walimchinja yule ng'ombe.



Noah alilia,
“Yule ng 'ombe alikuwa wa
mchungaji!”



Familia ilimpatia Noah bi
harusi.

